Mafunzo ya Kazi ya Kiufundi.
2023-2024

MEADOWDALE CTC

SAYANSI YA TIBA
Shiriki katika shughuli za kuvutia, unazofanya mwenyewe na kufanya kazi pamoja ili kupata masuluhisho ya shida halisi. Tumia utafiti wa kisayansi katika nyanja za mikrobiolojia, biokemia, ufundi wa chembe za urithi, maslahi ya matibabu, elimu ya kingamaradhi, na elimuadili ya kibiolojia. Boresha ujuzi wa maaraba kama vile majaribio, mbinu ya kuzuia bakteria, mbinu za biolojia ya molekuli, kutia na kuchuja viumbe hai kwenye bunguu la mwani, uchunguzi wa dalili muhumu.

BIASHARA - USAMBAZAJI WA BIDHAA
Wanafunzi watajifunza namna ya kuhamisha bidhaa kutoka kwa mtengenezaji hadi kwa mteja. Wanafunzi watasoma jinsi teknolojia inatumiwa kufuatilia bidhaa kupitia mifumo mbalimbali ya usambazaji na usafirishaji pamoja na namna ya kuboreshe mifumo inayotumiwa kusambaza bidhaa kwa wateja kwa gharama nafuu na kwa ufanisi.

USALAMA WA MTANDAONI
Tambua na kulinda mifumo ambayo imeunganishwa na mtandao dhidi ya mashambulizi ya mtandaoni. Buni na kuwezesha mitandao. Unganisha vifaa vya watumiaji pamoja na intaneti.

USANIFU WA KIDIJITALI
Gundua programu zinazowezesha uundaji wa mitindo bora ya usanifu ya sasa. Pata ujuzi wa kupiga picha za kidijitali kwa kufanya mazoezi halisi kwa kutumia vifaa bora zaidi. Jifunze jinsi ya kusanifu na kutengeneza tovuti za kisasa za majukwaa ya vifaa vya mkononi na kompyuta.

SAYANSI YA MAZOEZI
Gundua aina anuwai za taaluma za sayansi ya mazoezi, siha na tiba ya mwili. Jifunze jinsi ya kuzuia na kutibu vidonda kwa kutumia mbinu za kanuni za anatomia na fiziolojia. Wataalamu wa sayansi ya mazoezi wanahitajika
kushughulikia mahitaji ya jumla ya ustawi wa umma.

TEKNOLOJIA YA HABARI
Pata ujuzi muhimu wa dhana za kompyuta, ikiwa ni pamoja na maunzi na programu za kompyuta. Jifunze jinsi ya kusakinisha, kukarabati, na kutatua shida za mifumo ya maunzi ya kompyuta. Fanya mazoezi ya matengenezo ya kuzuia uharibifu. Sakinisha, usanidi na kutatua shida za maunzi na mifumo ya ziada ya mtandao.

KABLA YA UUGUZI
Kuza ujuzi wa kushugulikia wagonjwa walio na maradhi, waliojeruhiwa, au walemavu. Jiandae kufanya kazi hospitalini au katika vituo vya uuguzi chini ya uongozi wa wauguzi na madaktari. Gundua taaluma mbalimbali za tiba kupitia mazoezi ya maabara, kliniki, na kozi zinazohusiana. Kuza maadili ya kazi ya utaalamu na mawasiliano na ujuzi wa kushugulikia mgonjwa.

USANIDI WA PROGRAMU NA USANIFU WA MICHEZO
Jifunze jinsi ya kuunda programu rahisi za mwingiliano wa watumiaji. Jiandae kusanifu na kusanidi michezo kwa kutumia programu zinazouzwa na zinazopatikana kwa umma. Jifunze miundo ya lugha ya usanidi ya kiwango cha sekta ili kuandika programu zinazojumuisha madarasa, mbinu za darasa na matukio ya darasa.
Jifunze jinsi ya kushughulikia mbinu ya maingizo, uhuishaji, utambuzi wa mgongano na fizikia ya mchezo.

CHUO CHA UALIMU MJINI
Gundua taaluma ya elimu na machaguo yanayohusiana ya taaluma katika mazingira ya mjini. Pokea mtazamo wa kina wa taaluma ya ualimu kupitia tajriba inayotokana na miradi na ufundishaji unaofaa kwa utamaduni.

STIVERS SCHOOL OF PERFORMING ARTS

SINEMA YA KIDIJITALI
Wanafunzi watajifunza hatua za kabla ya utayarishaji, utayarishaji na hatua za baada ya utayarishaji wa aina mbalimbali za filamu fupi. Wanafunzi watajifunza utaalamu wa kuhariri kwa ngazi ya juu, programu za athari maalum, na matumizi ya kamera ya HD.

UPIGAJI WA PICHA
Jifunze teknolojia ya kisasa na kuelewa sanaa bunifu na upigaji wa picha ndani ya studio. Pata msingi thabiti katika kozi ya dhana, ufundi na studio. Jifunze misingi ya chumba cha kawaida cha kusafishia picha na upigaji wa picha za kidijitali, uchapishaji, mwangaza wa studio, programu ya picha ya Adobe Creative Suite, na programu za wavuti.

USANIFU NA UTAYARISHAJI WA TAMTHILIA
Programu hii inashughulikia mafunzo ya kubuni na kutayarisha vipengele vya kiufundi kwa taaluma za sanaa za maonyesho. Mafunzo haya yanaandaa wanafunzi kufanya kazi tofauti, kama vile: kufanya kazi kwenye maonyesho ya Broadway, kufanya kazi katika idara za sanaa za filamu na televisheni, kusimamia matukio makubwa, na ziara za maonyesho ya muziki.

PONITZ CTC

UTAALAMU WA TIBA

Kuza ujuzi wa kushugulikia wagonjwa walio na maradhi, waliojeruhiwa, au walemavu. Jiandae kufanya kazi hospitalini au katika vituo vya uuguzi chini ya uongozi wa wauguzi na madaktari. Gundua taaluma mbalimbali za tiba kupitia mazoezi ya maabara, kliniki, na kozi zinazohusiana. Kuza maadili ya kazi ya utaalamu na mawasiliano na ujuzi wa kushugulikia mgonjwa.

TEKNOLOJIA YA MAGARI

Tambua kasoro, ukague na kukarabati aina mbalimbali za magari. Tumia vifaa vya hali ya juu vya uchunguzi wa kutambua kasoro ili kutatua na kukarabati mifumo changamano ya magari huku ukijifunza ujuzi wa huduma kwa wateja.

BIOTEKNOLOJIA

Gundua jinsi viumbe hai kama vile seli, miti, na wanyama vinaweza kutumiwa kutatua matatizo ya maisha yanayohusiana na uhalifu, njaa, mazingira, lishe na afya. Tumia utafiti wa kisayansi katika nyanja za famasia, ubora wa maji, sayansi ya uchunguzi, tiba, botania, utafiti, sayansi ya chakula, na mikrobiolojia. Boresha ustadi wa maabara kama vile kupima vioevu, mbinu ya kuzuia bakteria, umwagiliaji, kutia na kuchuja viumbe hai kwenye bunguu la mwani.

BIASHARA - FEDHA

Pata maarifa ya msingi ya ulimwengu wa biashara, ikiwa ni pamoja na uchumi, kumiliki na kuendesha biashara, utandawazi, masoko, na kupanga fedha za kibinafsi. Jifunze na kutumia teknolojia muhimu ya biashara na programu ili kupata vyeti vya utaalamu vya Microsoft Office Specialist. Kuza ufahamu wa kazi na ujuzi unaohusiana ili kufanya uchaguzi wa kazi na uwe na uwezo wa kuajiriwa katika taaluma mbalimbali za biashara. Buni na kutekeleza uuzaji imara na mipango ya usimamizi ya kutatua changamoto halisi za biashara.

TEKNOLOJIA YA UJENZI

Jifunze misingi ya useremala, ikiwa ni pamoja na kuunda, kuweka madirisha na milango, ngazi, na paa. Wanafunzi pia watajifunza usanifu unaowezeshwa kwa programu za kompyuta na kukuza ujuzi wa kuunda mitindo mipya na urekebishaji.

SAYANSI YA VIPODOZI

Programu hii imeundwa kwa mujibu wa Bodi ya Jimbo ya Sayansi ya Vipodozi. Mwanafunzi lazima amalize mafunzo ya saa 1500 shuleni ili aweze kuhitimu kufanya Mtihani wa Jimbo wa Kukabidhiwa Leseni.

HAKI YA JINAI

Wanafunzi watashiriki katika shughuli za kufanya wenyewe katika taaluma ya haki ya jinai. Wanafunzi watajua jinsi ya kufunga pingu, kuhifadhi silaha, na kuondosha magari, ikiwa ni pamoja na matumizi ya nguvu.

SANAA ZA MAPISHI

Pika vyakula vya kitaalamu, keki, na vitobosha ukitumia wasilisho la kisanii. Panga, tayarisha na upakue vyakula kwa ajili ya milo ya kawaida na matukio makubwa. Kuwa sehemu muhimu ya timu inayopika milo kamili na uzoefu wa kipekee wa kula vyakula.

USAIDIZI KATIKA HUDUMA ZA MENO

Pata ujuzi muhimu wa kuwasaidia madaktari wa meno na wataalamu wa usafi kuhudumia wagonjwa, kufanya majukumu ya ofisini, na majukumu ya maabara. Jifunze elimu ya afya ya kinywa ya mgonjwa, kuchanganya nyenzo za tiba ya meno, kuingiza mwanga, kutengeneza na kuweka eksirei za mdomo, udhibiti wa maambukizi, kuua vijidudu na huduma za usaidizi katika tiba ya upasuaji ya meno na matibabu ya dharura ya meno. Jifunze taratibu za jumla za ofisi, kuhifadhi rekodi za wagonjwa, na kubuni chati za afya ya meno.

TEKNOLOJIA ZA UHANDISI

Huwatayarisha wanafunzi kuwa viongozi wabunifu na wenye tija kwa kutumia kanuni za uhandisi, hisabati, na ustadi wa umakinifu. Wanafunzi huonyeshwa mbinu za uhandisi na kujifunza ujuzi wa mahitaji makubwa ya uchumi wa dunia.

SANAA YA PICHA NA USANIFU

Chunguza vipengele vyote vya tasnia ya mawasiliano ya picha. Kuza ujuzi katika usanifu wa kompyuta, upigaji wa picha, uchapishaji wa skrini, na kuchapisha matoleo ya kidijitali na yenye maumbizo makubwa.

SANAA ZA VYOMBO VYA HABARI

Wanafunzi hujifunza misingi ya utayarishaji wa utangazaji katika sauti, video, na uuzaji wakitumia studio ya runinga iliyo na vifaa vyote, chumba maalum cha kuhariri video, studio ya FM, na vibanda vya utayarishaji wa sauti. Mpango huu umebuniwa makusudi kukuza ujuzi ili wanafunzi waweze kuunda vipengee vya video na sauti peke yao kwa ajili ya utangazaji. Wanafunzi wataimarisha uwezo wao wa ubunifu na kugundua dunia kwa mtazamo wa vyombo vya habari.

TEKNOLOJIA YA FAMASIA

Chunguza kanuni tofauti za dawa, dhana za kazi, na ujuzi unaohitajika ili kuwa fundisanifu wa famasia. Wanafunzi watajifunza jinsi ya kusoma, kufasiri, na kutoa dawa. Watajifunza jinsi dawa huainishwa na kutolewa. Wanafunzi watajifunza athari za dawa katika mifumo tofauti ya mwili, mwingiliano wa dawa, athari na ufanisi kulingana na kipimo.

Dayton Public Schools haibagui kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, ulemavu au umri katika kushiriki kwenye mpango au shuguli yoyote. Kutokuwa na ufasaha wa lugha ya Kiingereza hakutakuwa kizuizi kwa uandikishaji na ushiriki katika programu za elimu ya ufundi wa kitaaluma.